**Maelezo**. Huku mwanga wa dunia unavyoelekezwa katika Mashariki ya Kati, tunaona kwa uwazi utata huu ukiongezeka. Mabishano haya juu ya Sayuni yataendelea kuongezeka kwa nguvu hadi mwisho.

7. Je! Nabii Obadia ametufahamisha nini pia kuhusu pambano hili na matokeo ya mwisho? Obadia 1:15-18.
8. Je! Kwa nini malipo haya ya uharibifu yalinenwa juu ya watu hawa? Kosa lao lilikuwa lipi? Obadia 10, 11, 13.

**Maelezo**. Kauli hiyo imesemwa katika Obadia 15, "Kama ulivyofanya, na wewe utatendewa vivyo hivyo." Nchi za Mataifa leo zimeacha na kukaa mbali sana na njia ya haki, kama Wayahudi walivyowahi kufanya. Wanafanya makosa yale yale dhidi ya mbinguni na kwa hivyo watapata maafa kama hayo.

9. Je! Nabii Zekaria alisema nini pia kuhusu wakati huu? Mataifa yatamzingira nani? Zekaria 12:2.
10. Je! Ni nini kitakachokuwa jiwe lenye kulemea, na ni nini kitakachotokea kwa mataifa fulani yanayolemewa nalo? Zekaria 12:3.
11. Je! Ni nini kilichosemwa juu ya wakuu wa Yuda, wakati huu? Zekaria 12:6.



8. Ni nini ilisemwa kuhusu Israeli kuitia nchi uchafu, na kuhusu adhabu yao kwa ajili ya dhambi zao? Ezekieli 36: 17-20.
9. Je, Baba alikuwa na huruma juu ya Israeli, na ni baraka wakati huu kuwakusanya Wayahudi tena Israeli, ni kwa ajili ya haki yao wenyewe? Ezekieli 36:22, 32
10. Kutakuwa na mabaki ya watu hawa yaliyotengwa kwa ajili ya matumizi takatifu (kutakaswa), na ni jinsi gani kazi hii ilikuwa iaanze nao? Ezekieli 36: 23, 24; Warumi 9:27, 28.
11. Baba anasema nini kuhusu umiliki wa ardhi ambapo sasa wanakusanywa? Je, hii ardhi ni ya Israeli? Ezekieli 36:24.
12. Nyoyo zao zitabadilishwa kutoka kwa nyoyo za jiwe wawekwe nyoyo za nyama kabla kukusanywa au ni baadaye? Ezekieli 36:24-27.
13. Ni vipi kuhusu baraka juu ya nchi katika kuifanya iwe na mazao, na hii itakuwa na athari juu ya watu katika kukumbuka dhambi zao, na matendo yao maovu? Ezekieli 36:30, 31
14. Katika siku ile wao watakuwa wanatakaswa maovu yao, kupitia kupokea Roho, watakuwa wakijenga mahali palipoharibiwa na miji ya kale, na nchi itafanana na bustani la Edeni? Ezekieli 36:33-36.



10. Je! Washindi watakuwa wameandika jina gani jipya juu yao? Ufu. 3:12.
11. Ni hatima gani mbaya inayowangoja wote wanaoondoa au kuongeza unabii wa kitabu hiki? Ufu. 22:18, 19.
12. Ni sifa gani zinazohitajika ili kuingia katika Jiji hili? Ufu 22:14.
13. Ni nini kitakachoangazia Jiji hili zuri? Ufu. 22:5; 21:23, 25.
14. Ni nani anayetualika kwa upendo, ili tuwe na sehemu katika Jiji hilo? Ufu. 22:16, 17.
15. Je, Yohana alikiona kiti cha enzi cha Elohim, na kilikuwa wapi? Ufu. 22:3.
16. Je! Ni nini kitakachotokea kwa huzuni, maumivu na kuteseka kote wakati huo? Ufu. 21:4, 5.

******************************



***"Utakieni Yerusalemu amani; Na wafanikiwe wakupendao" Zaburi 122:6***



# Masomo Ya Bibilia

***kwa***

**KANISA LA ELOHIM (COG)**
**Siku Ya Saba (7th day)**

Robo Ya Nne
2022

Ya
Oktoba, Novemba, Desemba.
**(Tishrei, Cheshvan, Kislev, Tevet)**

Watenda kazi wanahitajika,
Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache...

**Tuma maombi yote kwa S.L.P 568, Jerusalem — Israel**

15. Ni tukio gani Mtume Paulo alishirikisha na kupokelewa kwa Israeli tena? Warumi 11:15-21.

******************************

**Somo la Oktoba 29, 2022 (Cheshvan 4, 5783)**

## UZAO WA KIFALME WA YUDA

**Somo Kuu: Zekaria 12.**
**Fungu La Kukariri: Zekaria 13:1.**

1. Je! Ni nini kilichotabiriwa katika unabii wa mapema zaidi kuhusu kabila la Yuda? Mwanzo 49:9,10.
2. Je! Musa alitabiri baraka gani kwa ajili ya Yuda? Kumbukumbu la Torati 33:7.
3. Ni nani alikuwa mfalme wa kwanza kutoka katika ukoo wa Yuda? 2 Samweli 2:4; 5:3-5.
4. Baadaye, kwa sababu ya dhambi, ni nini kingepata Yuda? Yeremia 13:19.
5. Je! Yuda wangekaa kwa uhamisho kwa muda gani? Danieli 9:2; Yeremia 25:11,12.
6. Je! Ni nini kilichotabiriwa zamani sana kuhusu hatima ya mwisho ya Yuda? Zekaria 2:12,13.
7. Agano jipya linafanywa na nani? Yeremia 31:31-37.
8. Je! Ni unabii gani wa nyakati za mwisho tunaopata katika Zekaria 12?
9. Je! Mfalme Yahshua alitoka katika kabila gani? Waebrania 7:14.



Daniel yalitimia. Sasa tuko katika wakati wa marejesho ya mwisho ya Israeli kwa Nchi yao ya Ahadi, ambayo inatupatia mpangilio wa kuja kwa Masihi kama Mfalme.

******************************

**Somo la Desemba 10, 2022 (Kislev 16, 5783)**

## UTATA JUU YA SAYUNI

**Somo Kuu: Isaya 34:1-8; Yeremia 25:30-38**
**Fungu La Kukariri: Isaya 34:8**

1. Nabii anazungumza na nani, na onyo hilo ni la jumla kiasi gani? Isaya 34:1.
2. Je! Ni nini kitakachotokea kwa majeshi yote ya dunia? Isaya 34:2.
3. Katika kipindi hiki cha uharibifu, au karibu na mwisho wake nini kilichosemwa kuhusu majeshi ya mbinguni? Isaya 34:4. Linganisha na Ufunuo 6:13, 14.
4. Je! Ni nini kilichosemwa kuhusu kuangamizwa kwa Idumea (Edomu) au wazao wa Esau? Isaya 34:5.
5. Nabii anatuambia nini zaidi kuhusu uharibifu wao na nchi kulowekwa katika damu? Isaya 34:6, 7. Linganisha na Ufunuo 14:19, 20.
6. Nabii anatujulisha nini kuhusu sababu ya wakati huu wa kutisha wa uharibifu, katika uhusiano wake na Sayuni? Isaya 34:8.



**Somo la Oktoba 1, 2022 (Tishrei 6, 5783)**

## ISRAELI SHAHIDI WA BWANA

**Somo Kuu: Hesabu 23.**
**Fungu La Kukariri: Isaya 43:12.**

1. Je! Hatima ya mwisho ya lsraeli ni gani? Kutoka 19:6.
2. Je, Waisraeli walikusudiwa kuunganishwa na mataifa au watabaki pekee yao? Kumbukumbu la Torati 33:28; Hesabu 23:9.
3. Je, Bwana aliiweka mipaka ya Israeli tangu awali? Kumbukumbu la Torati 32:8; 2 Samweli 7:10.
4. Katika hali ya dhambi, ni nini kingetokea kwa Israeli? Yeremia 30:11.
5. Je, taifa la Israeli lingeangamizwa milele? Yeremia 31:33.
6. Je! Watu wana maoni gani kuhusu Israeli? Yeremia 33:24.
7. Jibu ni gani? Yeremia 31:35-37; 33:25,26.
8. Baada ya kuadhibiwa, ni nini ambacho hatimaye kitawapata Israeli? Yeremia 33:7-9.
9. Ni ahadi gani za Abrahamu zitatimizwa wakati huo katika Israeli? Yeremia 33:14-16.
10. Je! Agano jipya litafanywa na watu gani? Yeremia 31:31-34.
11. Je! Ni mfalme gani atakayetawala juu ya Israeli takatifu? Luka 1:30-33; 22:29,30.



**Somo la Desemba 31, 2022 (Tevet 7, 5783)**

## MJI MTAKATIFU - YERUSALEMU MPYA

**Somo Kuu: Ufunuo Sura ya 21.**
**Fungu La Kukariri: Ufu 21:2.**

1. Je! Ibrahimu alikuwa akitafuta nini alipokuwa anakaa katika nchi ya Ahadi? Waebr. 11:8-10.
2. Ingawa tunakiri kwamba sisi ni wageni na wasafiri, ni nini hasa tunatangaza? Waebr. 11:13-16.
3. Ni kwa njia gani ya ajabu ambayo Mtume Paulo anatuambia kile ambacho WaMasihi waliozaliwa mara ya pili wamefikia, na ambapo majina yao yameandikwa? Waebr. 12:22-24.
4. Je! Yahshua alisema nini kuhusu makao ya Baba Yake (Yerusalemu Mpya)? Yohana 14:2, 3.
5. Je, tutapanda kwenye majumba haya, au majumba haya yatashuka duniani? Ufu. 21:2, 10.
6. Ni jinsi gani dunia itasafishwa na kurekebishwa kabla ya jiji hilo lenye kupendeza —Yerusalemu Mpya — kushuka? 2 Petro 3:10-13.
7. Unabii huo utakapotimizwa, je, kutakuwa na bahari tena? Ufu. 21:1.
8. Baada ya dunia kufanywa kuwa mpya, je, tutakuwa na kumbukumbu zozote zenye kuhuzunisha? Isa. 65:17.
9. Paulo anatofautishaje Yerusalemu ya siku hii na ile itakayoshuka kutoka Mbinguni? Wagal. 4:25, 26.

7. Je! Waliruhusiwa pia kuchukua vyombo vilivyohitajika kwa nyumba ya Elohim? Mstari wa 19.
8. Je! Kulikuwa na vyombo vya maana vilivyochukuliwa kutoka Nyumba ya Elohim ya kwanza, ambavyo viliharibiwa na Nebukadreza, Mfalme wa Babeli? 2 Mambo ya Nyakati 36:18; Danieli 5: 1-5.
9. Artashasta alitoa amri gani juu ya kutoa pesa kwa kazi hii kubwa? Ezra 7:21.
10. Kulingana na tarehe iliyo juu ya ukurasa wa Bibilia yako, amri hii ya Artashasta ilitoka mwaka gani? (Bibilia nyingi zina tarehe hizi katika pembeni na zote zinaonyesha tarehe ya 457B.C.).
11. Je! Ni muda gani baada ya hii amri, upatanisho ulifanywa kwa sababu ya uovu? Danieli 9:24; Mathayo 26: 6-13.

**Maelezo**: Kuanzia tarehe ya juu ya ukurasa katika bibilia yako utaona kwamba tarehe ya kusulubiwa imepeanwa kama 33 A.D. Kuongeza kwa idadi hii ya miaka 457 B.C (Ezra 7) wakati amri ilitoka na pesa zilipotengwa kwa ajili ya ujenzi wa Hekalu, inafika siku 490 au wiki 70 tu. Maelezo kuu ya unabii huo yalitimizwa kwa ajabu sana. Masihi alikuja; akakatiliwa mbali; upatanisho ulifanywa kwa ajili ya dhambi; Mtakatifu, Masihi, alitiwa mafuta; jemadari (Tito Mrumi) aliyefuata baadaye, akauangamiza mji; ukiwa ukawa juu ya Ardhi Takatifu. Matangazo yaliyotolewa na Gabrieli kwa



10. Malaika alipomtokea Mariamu, ni unabii gani uliotolewa? Luka 1:31-33.
11. Maneno mazuri ya kinabii, yaliyoandikwa katika nyakati za Agano la Kale, yanayohusu kuzaliwa kwa Masihi yanapatikana katika Mika 5:2 na Isaya 9:6,7.
12. Je! Ni nini kilichoandikwa katika kitabu cha Danieli kuhusu Ufalme? Danieli 2:44.

**Maelezo**. Tumegusia maneno machache tu kati ya unabii mwingi muhimu kuhusu Yuda. Yote yanaelekeza kwa Masihi na Ufalme ujao.

*******************************

**Somo la Novemba 5, 2022 (Cheshvan 11, 5783)**

## ADHABU YA ISRAELI NA KUREJESHWA KWAO

**Somo kuu: Walawi 26:1-31.**
**Fungu la kukariri: Luka 21:24.**

1. Je, ni baraka gani na ni ulinzi gani Israel waliahidiwa ikiwa watamtii Elohim? Walawi 26:3-12.
2. Ikiwa watashindwa kumtii, adhabu yao ingekuwa gani? Mistari 14-17.
3. Ni kwa muda gani wataadhibiwa? Mstari 18.
4. Je, ni maonyesho gani yanaonyesha ukali wa hukumu ya Elohim dhidi yao? Mithali 19, 21, 24, 28.



**Maelezo**. Hii ni mara ya pili kwa watu hawa kukusanywa kurudi katika nchi yao. Mara ya kwanza walipokusanywa kutoka Babiloni, lakini sasa ni kutoka pembe nne za dunia. Wakati huu wa sasa kuna Wayahudi ambao wanatoka katika mataifa 74 tofauti.

8. Elohim atakapomaliza kuwakusanya Wayahudi kutoka mataifa yote, je, mioyo yao itabadilika? Ezekieli 36:24-26.
9. Watakusanywa katika nchi gani na je, Elohim anafanya hivi kwa ajili yao? Mistari 28:32.
10. Upofu huu utaondolewaje? Yeremia 23:3,4; 3:14,15.

**Maelezo**. Macho ya vipofu ya Mataifa yalifunguliwa kwa wajumbe wa nuru waliotumwa kwa mataifa yote, vivyo hivyo wachungaji wanapaswa kuwafundisha Israeli nuru ya kweli, na uweza wa Roho Mtakatifu.

11. Baada ya kukusanywa kwao kukamilishwa, mataifa watafanya nini? Yoeli 3:1; 9-12.
12. Je! Tokeo la mwisho la matukio hayo litakuwa nini? Yoeli 3:2, 16-21.

******************************



12. Waliokombolewa na Bwana wataingia kwa malango ya mji. Ni majina gani yataandikwa juu ya milango? Ufunuo 21:12; Ezekieli 48:31-35; (Angalia pia Wagalatia 3:29 na Mwanzo 12:3).

*******************************

**Somo la Oktoba 8, 2022 (Tishrei 13, 5783)**

## YERUSALEMU NA MLIMA SAYUNI

**Somo Kuu: Isaya 62: 1-12.**
**Fungu La Kukariri: Zaburi 102: 16.**

1. Wakati tarumbeta ya malaika wa saba itakaposikika, sauti kubwa kutoka mbinguni itatangaza nini? Ufu. 11:15.
2. Ni nani atakayemsaidia Mwokozi na Mfalme katika ufalme huu mpya? Ufu. 20: 4; pia Ufu. 2: 25-27.
3. Watakaoshinda watatawala wapi na Mfalme? Je, itakuwa Mbinguni au hapa duniani? Ufu. 5: 9, 10.
4. Je, ni mahali gani hapa duniani ambapo kutakuwa makao makuu ya Ufalme? Zaburi 110: 2; Zak. 1:17; pia 2:12, 13.
5. Je, ni nini kitatokea kwa wafalme waovu, na mataifa ambayo hayatatumikia Mfalme wetu, wakati wa mamlaka ya fimbo ya chuma? Zaburi 110: 2; Zak. 14: 9.

**Maelezo.** Kutumika kwa maneno **"Mara saba"** kwa mara nyinngi hakumaanishi mara saba. **"Saba"** katika maandiko inamaanisha ukamilifu wa adhabu yao; basi hii inatumika kuonyesha mkazo, Ukamilifu wa kuadhibiwa kwao. Mara saba (siku moja kwa mwaka - Ezekieli 4:5, 6) au 2,520 pamoja na uhamisho wa Babeli chini ya Nebkadineza mwaka wa 486 B.C., na iliishia na uokoaji wa Waturuki chini ya Jenerali Allenby katika vita vya kwanza vya dunia, mwaka wa 1914.

5. Kwa kipindi cha miaka mingi ni nini ilisemwa kuhusu ardhi yao? Walawi 26:31-35.
6. Adhabu hii kali itawasababisha wafanye nini? Mstari 28, 29.
7. Je, ni maonyesho gani mengine yanaonyesha ukali wa adhabu yao? Yeremia 31:27, 28.
8. Katika hii miaka ya uhamisho, walikuwa aje mbele za Elohim? Mstari 35-37.
9. Je, ni nini ilisemwa kuhusu utambulisho wao miongoni mwa mataifa katika kipindi hiki? Isaya 61:9
10. Je, maana hasa ya taabu hii ni nini? Hosea 5:15.
11. Kwa nini Elohim hakuwaharibu kabisa katika hii miaka? Walawi 26:44, 45.
12. Je, ni unabii gani wa Daudi unatimizwa sasa? Zaburi 102:15, 16.

*******************************



**Maelezo**. Yerusalemu leo ni jiji la ajabu la kisasa, ambalo limejengwa kwa miaka mingi tangu Wayahudi waliporudi.

*******************************

**Somo la Desemba 3, 2020 (Kislev 9, 5783)**

## UNABII KUHUSU YERUSALEMU

**Somo Kuu: Ezra 7.**
**Fungu La Kukariri: Ezra 7:27.**

1. Wakati malaika Gabrieli alipomtembelea Danieli huko Babeli, kusudi lake kuu na ujumbe wake ulikuwa ni upi? Danieli 9:24 na sehemu ya kwanza ya aya ya 25.
2. Je! Ni tukio gani lingine muhimu kuhusu Masihi ambalo malaika Gabrieli alimjulisha? Mstari wa 26 (sehemu ya kwanza).
3. Je! Amri ilitoka ili kujenga tena nyumba ya Elohim? Ezra 7: 13,20.
4. Je! Hizi fadhili na maagizo zinapatikana katika barua ya Mfalme kuhusu jambo hili? Mstari wa 11.
5. Je! Kulikuwa na upeanaji wowote wa fedha na dhahabu uliopewa Ezra, kuhani mkuu wa Wayahudi? Mistari 15,16.
6. Je! Wayahudi waliruhusiwa kununua, na kuchukua kwenda Yerusalemu, mahitaji mengi? Mstari wa 17,18.



6. Je, Yerusalemu itafanywa kuwa sifa duniani kwa kazi ya maandalizi ya Mfalme anayekuja? Isa. 62: 6, 7.
7. Ni nini kilichosemwa juu ya malipo, na atakuwa na kazi mbele yake ya kufanya baada ya kuja? Isa. 2: 4; 1 Wakor. 15: 25-28.
8. Je, ni nini kinachosemwa juu ya wakati uliowekwa wa kuirehemu Sayuni? Zaburi 102: 13.
9. Kufuatia wakati huu uliowekwa, Je Sayuni itajengwa kabla Mfalme kurudi? Zaburi 102: 14-16.
10. Je, itakuwa matajiri au watu ni masikini ambao watatumainia Sayuni na kuipenda? Isaya 14:32.
11. Ni nini kinachosema juu ya wale wanaochukia Sayuni, na wale husahau Mlima Wake Mtakatifu? Zaburi 129: 5; Isa. 65:11, 12.
12. Je! Bwana huwa na wivu sana kwa Sayuni, na ina nafasi maalum kwake Yeye, na kwa watu Wake? Zak.1: 14; Zaburi. 53: 6.

*******************************

**Somo la Oktoba 15, 2022 (Tishrei 20, 5783)**

## WAYAHUDI KATIKA NCHI TAKATIFU

**Somo Kuu: Ezekieli 38:14-23.**
**Fungu La Kukariri: Ezekieli 38:16.**

1. Ni baraka gani maalum ambazo Bwana aliahidi kwa Ibrahimu na kwa uzao wake? Ni nini



sehemu gani ya ono hilo ambayo bado itakuwa katika wakati ujao? Kifungu cha 44, 45.

*******************************

**Somo la tarehe 24 Desemba 2022 (Kislev 30, 5783)**

## MWISHO WA NYAKATI ZA MATAIFA

**Somo Kuu: Luka Sura ya 21.**
**Fungu La Kukariri: Luka 21:15.**

1. Je! Wayahudi wangetawanyika kati ya mataifa yote kwa muda gani? Luka 21:24.
2. Je! Kupungua huku kwa Wayahudi kungeleta nini kwa Mataifa? Warumi 11:12.
3. Je! Upofu huu ungekuwa juu ya macho ya Yuda kwa muda gani? Warumi 11:25.
4. Wakati huu wa kutawanywa kwa Yuda, ni nini kilichosemwa kuhusu nchi zote za Mataifa? Mathayo 24:14.
5. Ahadi zimetolewa kwa nani? Wagalatia 3:16. Na watu wa mataifa mengine wanashirikije katika ahadi hizo? Warumi 11:24.
6. Kupungua kwa Wayahudi kulileta utajiri kwa watu wa mataifa mengine, je, kupokewa kwao kutaleta nini? Kifungu cha 15.
7. Kukusanywa tena kwa Yuda kutakuwa pana kiasi gani, kabla ya baraka hizo kuja? Isaya 11:11,12.

2. Je, wakati ungefika, hata hivyo, ambapo Bwana angewarudisha tena katika nchi yao wenyewe? Yeremia 32:37.
3. Bwana alipoleta mabaya juu yao, je, aliahidi vivyo hivyo kuwabariki katika siku za mwisho? Yeremia 32:41-44; Hosea 3:4,5.
4. Ni mfano gani hasa wa mchana na usiku ambao Elohim alifanya ili kuthibitisha kwamba Wayahudi wangekusanywa tena? Yeremia 31:35-37.
5. Je! Nabii Yoeli anathibitisha nini pia kuhusu baraka za Yuda katika siku za mwisho? Yoeli 3:6,7.
6. Jinsi gani kusanyiko la mwisho lingekuwa kubwa? Isaya 11:12.
7. Je, wakati wa mtawanyiko wao miongoni mwa Mataifa, walipoteza utambulisho wao, na hivyo wasitambuliwe kama watu? Isaya 61:9.
8. Je! Bwana atawarudisha katika nchi yao wenyewe kwa sababu ya wema wao, au ni kuthibitisha neno lake la hakika la unabii? Ezekieli 36:1-12,21-28.
9. Mtazamo wao utakuwaje kwa Elohim katika kukusanywa kwao tena siku za mwisho? Yeremia 31:6-11,23-28.
10. Tunajuaje kwamba unabii huo haurejelei kukusanywa tena kwa Wayahudi baada ya uhamisho Babiloni? Isaya 11:11; Yeremia 16:14-16.
11. Wakati wa kukusanywa tena, je, walipaswa kukarabati miji iliyoharibiwa ya kipindi cha hivi karibuni au ile iliyofanywa ukiwa miaka mingi iliyopita? Isaya 61:4.



**Somo la Novemba 12, 2022 (Cheshvan 18, 5783)**

## KUJUMUISHWA KWA MATAIFA KATIKA JAMII YA ISRAELI

**Somo Kuu: Warumi 11; Waefeso 2.**
**Fungu La Kukariri: Waefeso 2:12, 13.**

1. Wayahudi walikuwa na ziada gani juu ya mataifa mengine chini ya mbingu? Warumi 3:1, 2; 9:4, 5; Yohana 4:22.
2. Je, Biblia inasemaje juu ya Mataifa? Waefeso 2:12.
3. Ni ahadi gani isiyo na dosari Elohim huwapa? Hosea 2:23; Isaya 62:2.
4. Katika utekelezaji wa ahadi yake kwa Mataifa, hali gani mbaya iliangukia taifa la Kiyahudi? Warumi 11:7-10.
5. Hali hiyo itawakumba hata lini? Isaya 6:11-13.
6. Ni matokeo yapi ya ajabu kutokana na kuanguka kwa taifa la Kiyahudi yako kwenye mataifa? Warumi 11:11, 25, 28, 30-33.
7. Ni nini imewezesha mataifa kupandikizwa katika jamii ya Israeli? Waefeso 2:11-14.
8. Wao sasa ni washiriki wa familia ya Ibrahimu na warithi? Wagalatia 3:26-29; Waefeso 3:5, 6; Warumi 10:12.
9. Ni onyo gani kali imetolewa kwa warithi wa kupandikizwa? Warumi 11:20-23.
10. Je, Mataifa waumini wanatarajiwa kufanya nini? 1 Petro 2:5, 9, 10.



2. Ufalme wa kwanza wa ulimwengu wote uliitwaje? Jina la mfalme wa kwanza lilikuwa gani? Danieli 2:1.
3. Walimwita nani hili kutafsiri ndoto hii? Danieli 2:2.
4. Je! Watu wenye hekima walimjibu nini mfalme? Danieli 2:10, 11.
5. Je! Danieli alifunuliwa ndoto hiyo kwa njia gani? Danieli 2:17, 19.
6. Je! Mfalme alisema nini kuhusu Danieli na rafiki zake? Danieli 1:19-24, 17.
7. Je! Ni kwa nini Bwana alimfunulia Danieli ndoto? Danieli 2:17, 18.
8. Baada ya Danieli kufunuliwa hiyo ndoto alifanya nini? Danieli 2:23.
9. Je! Mfalme Nebukadneza aliota ndoto gani? Danieli 2:31-38.
10. Ni nini kinachowakilishwa na kichwa cha dhahabu? Danieli 2:36-38.
11. Kama sanamu hii kuu iliwakilisha Utawala wa Mataifa juu ya ulimwengu, ni falme ngapi za ulimwengu wote zilipaswa kufuata ufalme wa Nebukadreza, kabla ya ufalme wa Elohim kusimamishwa? Mstari wa 39, 40.
12. Ili kuwakilisha hali dhaifu na isiyo imara ya ulimwengu wa Mataifa ulipokaribia mwisho wake, ni nini kilichosemwa juu ya miguu na vidole vyake vya miguu? Mstari wa 41-42.
13. Kwa kuwa falme hizi nne zimekuja kwa mpangilio wao ufaao kulingana na tangazo la Elohim, ni



kimeahidiwa kwa wale wanaowabariki watu waliochaguliwa na wale wanaowalaani? Mwanzo 12:1-3.

2. Ni jamii gani ya watu wanaoshikilia hati ya kisheria ya Nchi Takatifu? Mwanzo 15:18, 17:8.
3. Je, Elohim amewanyima warithi halisi wa mali hii? Yeremia 31:35-37; Warumi 11:1-4.
4. Ni nini kilichosemwa kuwahusu wanapokuwa kati ya mataifa? Isaya 61:9.
5. Je, Bwana anakusanya jamii ile ile ya watu kurudi kwenye Nchi ya Israeli ambayo aliiondoa katika nchi hio? Yeremia 32:37.
6. Je, Baba wa Mbinguni anawarudisha Wayahudi katika nchi yao wenyewe kwa sababu ya sifa zao wenyewe, au kwa ajili ya jina Lake mwenyewe? Ezekieli 36:22.
7. Je, watapewa moyo na roho mpya? Aya 26. Je, imesemwa nini juu ya ukiwa na miji ya kale? Mstari wa 34-36.
8. Wakati nchi ya kaskazini na satelaiti zake zitakapokuja dhidi ya Yerusalemu, je, watakuwa watu wa Israeli (Wayahudi) katika nchi au ni jamii nyingine? Ezekieli 38:14,15.
9. Vita hivyo na uharibifu vitatukia lini, na ni dhidi ya nani? Kifungu cha 16.
10. Bwana anapokusanya mataifa ili kuhukumu mbele ya Yerusalemu, ni kabila gani la Israeli linalotajwa hasa kuwa lilikusanywa Yerusalemu? Yoeli 3:1-2.

11. Ni kwa njia gani hili tendo la ajabu la Elohim halichunguziki? Warumi 11:33-36.

*******************************

**Somo la Novemba 19, 2022 (Cheshvan 25, 5783)**

## UNABII KUHUSU WAKATI UJAO WA YERUSALEMU

**Somo Kuu: Isaya 62.**
**Fungu La Kukariri: Isaya 62:6, 7.**

1. Je, kutakuwa na kazi ya maandalizi huko Yerusalemu kabla ya Bwana kurudi katika utukufu? Isaya 62:10.
2. Je! Ni nini itakuwa ujumbe maalum kwa watu wa mabaki, "Binti Sayuni," kwa wakati huu? Kifungu cha 11.
3. Ni nini kinachosemwa hasa juu ya watu wanaoshiriki sehemu kubwa katika kazi hii ya matayarisho? Kifungu cha 12.
4. Biblia inasema nini kuhusu sauti itakayoinuliwa huko Yerusalemu na Israeli kabla ya kurudi kwa Bwana? Isaya 52:8-10.
5. Je! Nabii Mika alisema ni nini kingetokea Yerusalemu katika siku za mwisho? Mika 4:1, 2. **Maelezo**. Fungu la maneno "Siku za mwisho" halirejelei kamwe kipindi cha wakati wa baada ya kurudi kwa Bwana, lakini ni kipindi cha kabla ya kurudi kwake. Kwa hivyo, kila mmoja wa



manabii hawa anaeleza juu ya hali ya kutangulia kurudi kwa Mwokozi wetu.
6. Je! Daudi aliyetunga Zaburi alisema nini kuhusu Sayuni? Zaburi 2:6-9; 110:2, 3.
7. Kiti cha enzi cha Mfalme Daudi kilikuwa Yerusalemu. Masihi, Mfalme wetu anayekuja, atatawala ulimwengu kutoka wapi? Isaya 9:7; Mika 4:7.
8. Je! Ni nini kilichosemwa kuhusu jua na mwezi Yerusalemu itapokuwa jiji kuu la ulimwengu? Isaya 24:23.
9. Je! Ni nini kilichosemwa zaidi kuhusu Yerusalemu? Isaya 33:20-22.
10. Bwana wetu atatawala katika Yerusalemu mpaka lini? Je, kazi Yake itakuwa gani? 1 Wakorintho 15:22-26.

*******************************

**Somo la Novemba 26, 2022 (Kislev 2, 5783)**

## UMUHIMU WA UNABII KATIKA UHAMISHO WA WAYAHUDI

**Somo Kuu: Isaya 62.**
**Fungu La Kukariri: Isaya 62:6, 7.**

1. Kwa sababu ya kosa, ni amri gani ambayo Elohim alitangaza dhidi ya taifa la Kiyahudi? Yeremia 29:18,19.



11. Zekaria anashirikisha kabila gani na Yerusalemu wakati Bwana atapigana kwa ajili ya Israeli? Zekaria 12:2,3.

*******************************

**Somo la Oktoba 22, 2022 (Tishrei 27, 5783)**

## UJUMBE KWA MILIMA YA ISRAELI

**Somo Kuu: Ezekieli 36**
**Fungu La Kukariri: Ezekieli 36:24.**

1. Ni kwa nani ujumbe huu hasa ulitumwa? Ezekieli 36: 1.
2. Maadui walisema nini kuhusu milima ya Israeli? Ezekieli 36:2.
3. Huu ujumbe ni wa wakati wetu kufuatia kipindi cha ukiwa, au ni kwa muda katika siku zilizopita? Ezekieli 36: 3.
4. Huu ujumbe ni upi kwa milima ya Israeli? Ezekieli 36:4-7.
5. Ahadi kwa milima ya Israeli kwa wakati huu, na siku za usoni ni zipi? Watu watamiliki nini kutoka kwa hiyo milima? Ezekieli 36: 8-10.
6. Ni nini imesemwa kuhusu jinsi Israeli wanavyofanyiwa wakati huu? Watatendewa sawa kama mbeleni au bora? Ezekieli 36:11.
7. Nchi hii itawahi kuwa ukiwa tena? Ezekieli 36:12.



**Maelezo**. Kutakuwa na sehemu ya Yuda itakayookolewa, hata hivyo, kabla ya matukio haya ya mwisho kutokea kama tunavyoelezwa katika Mstari wa 7, mnyonge zaidi kati ya watu jasiri ambaye alitoka kwa ushujaa dhidi ya jitu la Wafilisti, Goliathi na kumuua kwa kombeo, na jiwe alilokota katika kijito. 1 Samweli 17:20-50. Tunaona ni vivyo hivyo leo hapa katika Israeli kama nabii huyu alivyosema. Wayahudi hawaogopi Waarabu milioni mia wanaowazunguka, ingawa wanapewa silaha na Urusi na mataifa mengine. Wanapoulizwa kuhusu hali hiyo, wao husema, "Tunamwamini Elohim." Hatuna hofu na Waarabu.
12. Je! Matokeo ya mwisho ya mapambano hayo yatakuwa nini? Zekaria 9; Yoeli 3:1, 2, 16; Zekaria 14:1-3.

*******************************

**Somo la Desemba 17, 2022 (Kislev 23, 5783)**

## ISHARA KUU YA NYAKATI ZA MATAIFA

**Somo Kuu: Danieli 2:20-45.**
**Fungu La Kukariri: Danieli 2:21.**

1. Je! Ndoto ya mfalme Nebukadreza na tafsiri yake ilikuwa nini? Danieli 2:31-44.